# IV.
# Financial Management

## Mada ya 40C

## Jinsi ya kutumia aina tofauti za rekodi

# JARIDA LA UHAKIKA

## IV. Financial Management

## Mada ya 40c: Jinsi ya kutumia aina tofauti za rekodi

### 1. Daftari ya fedha taslimu

Daftari hii huwekwa ili kurekodi **mapato na gharama katika fedha taslimu** Naira (N). Unaweza kutumia leja.

Ingiza habari katika njia ifuatayo:

- **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli ya biashara
- **Maelezo:** eleza bidhaa au huduma iliouzwa
- **Naira zilizoingia:** ingiza kiasi cha pesa kilichopokelewa
- **Naira zilizotoka:** ingiza kiasi cha pesa kilichotoka

| Tarehe | Maelezo | Naira zilizoingia | Naira zilizotoka |
|---|---|---:|---:|
| 04 Jan 2009 | Mauzo ya chupa mbili za Ultracide | N2,400 | |
| 05 Jan 2009 | Kununua kalamu na leja | | N1,500 |
| | | | |
| | | | |
| **JUMLA** | | **N2,400** | **N1,500** |

Tofauti baina ya Naira zilizoingia na Naira zilizotoka inaitwa **masalio**. Kiasi hiki chafaa kiwe kwenye sanduku lako la pesa taslimu. Katika mfano huu utakuwa na N900 (N2,400 - N1,500) katika sanduku lako la pesa taslimu.

## 2. Rekodi za ununuzi

Vyote ulivyonunua (gharama) lazima virekodiwe katika rekodi za ununuzi. Unaweza kutumia leja.

Ingiza habari katika njia ifuatayo:

- **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli ya biashara
- **Ilinunuliwa kutoka kwa:** ingiza jina la kampuni au mtu ambaye ulinunua bidhaa kutoka kwake
- **Maelezo:** eleza bidhaa ulizonunua, pamoja na kiasi
- **Kiasi jumla ulichonunua:** ingiza kiasi jumla ulicholipa
- **Mtindo/namna ya kulipa:** eleza jinsi ulivyolipa. Kama ulilipa kwa kutumia hundi, ingiza nambari ya hundi hiyo. Kama ulilipa kwa kutumia pesa taslimu, lazima pia uingize shughuli hii ya kibiashara kwenye daftari ya fedha taslimu!

| Tarehe | Ilinunuliwa kutoka kwa | Maelezo | Kiasi jumla cha vilivyononunuliwa | Namna/mtindo wa kulipa |
|---|---|---|---|---|
| 02 Jan 2009 | Isaac & Co | Sacheti 80 za Aldrex | N8,000 | Hundi (nambari 039) |
| 05 Jan 2009 | Pat's bookshop | Kalamu 5 na leja 2 | N1,500 | Pesa taslimu |
| 05 Jan 2009 | Golden Inputs | Chupa 100 za Ultracide | N120,000 | Muamana |
| | | | | |
| | | | | |
| **JUMLA YA UNUNUZI WA MWEZI WA JANUARI 2009** | | | **N129,500** | |

Sasa unaweza kukokotoa kiasi ulichotumia kwa kila wiki, mwezi, au mwaka.

## 3. Rekodi za mauzo

Mauzo yako yote (mapato) yarekodiwe katika rekodi za mauzo. Unaweza kutumia leja.

Ingiza habari kwa njia ifuatayo:

- **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli za kibiashara
- **Maelezo:** eleza bidhaa ulizouza.
- **Ziliuziwa:** ingiza jina la kampuni au mtu uliemuuzia bidhaa
- **Bei ya kila moja ya bidhaa:** ingiza bei ya kila bidhaa moja
- **Kiasi:** ingiza nambari ya bidhaa ulizouza
- **Kiasi cha jumla:** ingiza jumla ya kiasi cha mauzo
- **Mtindo/namna ya kulipa:** eleza jinsi bidhaa zilivyolipwa. Kama zililipwa kwa kutumia hundi, ingiza nambari ya hundi hiyo. Kama zililipwa kwa kutumia pesa taslimu, lazima pia uingize shughuli hii ya kibiashara kwenye daftari ya fedha taslimu!

| Tarehe | Maelezo | Iliuziwa | Bei ya bidhaa moja (katika Naira) | Kiasi | Kiasi cha jumla (katika Naira) | Namna/mtindo wa malipo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 04 Jan 2009 | Ultracide | Bw. Adjei | N1, 200 | 2 | N2, 400 | Pesa taslimu |
| 04 Jan 2009 | Snipper | Bw. Adjei | N200 | 1 | N200 | Pesa taslimu |
| 05 Jan 2009 | Aldrex | Sam Kwagi | N100 | 15 | N1, 500 | Muamana |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| **MAUZO KWA JUMLA YA JANUARI 2009** | | | | | **N3,900** | |

Sasa unaweza kukokotoa kiasi ulichotumia kwa kila wiki, mwezi, au mwaka.

## 4. Rekodi za wadaiwa na waia

Maelezo ya jumla ya muamana huingizwa katika rekodi hizi. Unaweza kutumia leja.

Kwa bidhaa ulizonunua kwa muamana (inayomaanisha unadaiwa pesa na mtu fulani), ingiza habari katika njia ifuatayo:

- **Tarehe:** hii ndio tarehe ya kuingiza shughuli ya biashara
- **Jina la mwaia:** ingiza jina la kampuni au mtu aliyepeana muamana
- **Maelezo:** eleza bidhaa ulizonunua, pamoja na kiasi
- **Kiasi unachodaiwa:** ingiza kiasi kwa jumla ulichonunua
- **Kiasi ulicholipa:** Ingiza kiasi ulicholipa tayari
- **Masalio:** hii ni tofauti baina ya kiasi unachodaiwa na kile ulicholipa tayari

## Akaunti za kulipwa (Mwaia)

| Tarehe | Jina la mwaia | Maelezo | Kiasi unachodaiwa | Kiasi ulicholipa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 05 Jan 2009 | "Golden Inputs" | Chupa 100 za Ultracide | N120,000 | N50,000 | N70,000 |
| | | | | | |

Kwa bidhaa ulizouza kwa muamana (inayomaanisha unadai wateja pesa), ingiza habari katika njia ifuatayo:

- **Tarehe:** hii ndio tarehe ya kuingiza shughuli ya biashara
- **Jina la mdaiwa:** ingiza jina la mteja aliyenunua kwa muamana
- **Maelezo:** eleza bidhaa ulizouza, pamoja na kiasi
- **Kiasi unachodai:** ingiza kiasi kwa jumla kilichonunuliwa na mteja
- **Kiasi kilicholipwa:** Ingiza kiasi kilicholipwa na mteja tayari
- **Masalio:** hii ni tofauti baina ya kiasi unachodai mteja na kile alicholipa tayari

## Akaunti za kupokelewa (Wadaiwa)

| Tarehe | Jina la mdaiwa | Maelezo | Kiasi cha kudai | Kiasi kilicholipwa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 05 Jan 2009 | Sam Kwagi | Sacheti 15 za Aldrex | N1,500 | 0 | N1,500 |
| | | | | | |

# MAELEZO YA ZIADA

## IV. Financial Management

## Mada ya 40c: Jinsi ya kutumia aina tofauti za rekodi

**Vitu au vipengele kadhaa ni muhimu:**

| Mauzo | Ununuzi | Zilirekodiwa katika daftari ya fedha taslimu? | Zilirekodiwa katika rekodi za ununuzi? | Zilirekodiwa katika rekodi za mauzo? | Zilirekodiwa katika rekodi za wadaiwa na waia? |
|---|---|---|---|---|---|
| Kwa pesa taslimu | | Ndio | La | Ndio | La |
| Kwa muamana | | La | La | Ndio | Ndio |
| Kwa uhamisho wa pesa au hundi | | La | La | Ndio | La |
| | Kwa pesa taslimu | Ndio | Ndio | La | La |
| | Kwa muamana | La | Ndio | La | Ndio |
| | Kwa uhamisho wa pesa au hundi | La | Ndio | La | La |

### Muhtasari:

- Shughuli zote za pesa taslimu huandikwa katika daftari ya fedha taslimu.
- Shughuli zote za muamana huandikwa katika rekodi za wadaiwa na waia.
- Ununuzi wote, bila kuzingatia mtindo/namna ulivyolipiwa, huandikwa katika rekodi za ununuzi.
- Mauzo yote, bila kuzingatia mtindo/namna yalivyolipiwa, huandikwa katika rekodi za mauzo.

- Shughuli zote za kibiashara katika pesa taslimu au muamana huandikwa mara mbili. Shughuli za pesa taslimu huandikwa katika daftari ya fedha taslimu na katika rekodi za ununuzi (kama ni bidhaa zilizonunuliwa) au rekodi za mauzo (kama ni bidhaa zilizouzwa). Shughuli ya kibiashara kwa muamana huandikwa katika rekodi za wadaiwa na waia na katika rekodi za ununuzi (kama ni bidhaa zilizonunuliwa) au rekodi za mauzo (kama ni bidhaa zilizouzwa).
- Shughuli za kibiashara za kutumia uhamisho wa pesa au hundi huandikwa tu katika rekodi za ununuzi (kama ni bidhaa zilizonunuliwa) au rekodi za mauzo (kama ni bidhaa zilizouzwa).

# MWONGOZO

## IV. Financial Management

## Mada ya 40c: Jinsi ya kutumia aina tofauti za rekodi

**Vifaa vinavyohitajika:**

☑ Ubao ulio na makaratasi

☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)

☑ Copies of all visuals for all participants *(see Visuals)*

**Muda unaohitajika:** Dakiki 120

**Maandalizi:**

☑ Makaratasi yalio na fomu tupu zilichorwa kwazo

☑ Makaratasi yalio na maagizo yafuatayo: *(tumia karatasi moja kama daftari ya fedha taslimu, moja kama rekodi za ununuzi, na moja kama rekodi za mauzo)*

- Daftari ya fedha taslimu
  - 8 Jan 2009: Mauzo ya chupa mbili za Cypermethrin kwa bei ya N2,600
  - 9 Jan 2009: mauzo ya chupa moja ya Ultracide kwa bei ya N1,200
  - 9 Jan 2009: kununua kadi ya simu kwa bei ya N500
- Rekodi za ununuzi
  - 09 Jan 2009 kadi ya simu kwa bei ya N500 ililipwa kwa pesa taslimu kutoka kwa mchuuzi wa barabarani
  - 10 Jan 2009 chupa 20 Cypermethrin kwa bei ya N26, 000 kwa hundi (nambari 40) kutoka kwa Isaac&Co
  - 11 Jan 2009 chupa 10 za Ultracide kwa bei ya N12, 000 kwa muamana kutoka kwa “Golden inputs”
- Rekodi za mauzo
  - 8 Jan 2009: mauzo ya chupa 2 za Cypermethrin kwa bei ya N2, 600 kwa pesa taslimu kwa Bw. Nartey
  - 9 Jan 2009: mauzo ya chupa 1 ya Ultracide kwa bei ya N1,200 kwa pesa taslimu kwa Bw. Abdullai

- 10 Jan 2009: mauzo ya chupa 2 za Ultracide kwa bei ya N2, 400 kwa muamana kwa Bw. Weja

# Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Onyesha mifano tofauti ya rekodi (ishikilie juu) na uwaambie kwamba katika kipindi hiki, tutajadili *Jinsi ya kutumia hizi aina tofauti za rekodi* (**K**ichwa). |
| **K**usadikia: | Elezea uzoefu wako katika uwekaji wa rekodi. |
| **M**anufaa: | Kama una uwezo wa kutumia fomu hizi tofauti, unaweza kuzitumia kufanya maamuzi bora kuhusu biashara yako. Mwishowe, biashara yako itakua na utapata pesa zaidi. |
| **M**alengo: | Kueleza na kuonyesha aina tofauti za rekodi. |
| **M**welekeo: | Hatutashughulikia rekodi za bidhaa; hii itakuwa mada itakayofuata. Katika kipindi hiki, tutajadili daftari ya fedha taslimu, rekodi za ununuzi, rekodi za mauzo, na rekodi za wadaiwa na waia. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba tutajadili rekodi tulizozitambulisha katika kipindi kilichotangulia:
    a. Rekodi za daftari ya fedha taslimu
    b. Rekodi za ununuzi
    c. Rekodi za mauzo
    d. Rekodi za wadaiwa na waia
2. Tutaanza na **daftari ya fedha taslimu**. Sambaza picha ya *mfano wa daftari ya fedha taslimu*. Onyesha washiriki nguzo nyingi (wima) zilizo na vichwa. Uliza mtu kusoma kwa sauti vichwa hivyo (tarehe, maelezo, Naira zilizoingia, Naira zilizotoka). Uliza, kichwa baada ya kichwa, kama yeyote anaweza kutaja aina ya habari inayofaa kuingizwa hapa.
    - **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli ya biashara
    - **Maelezo:** eleza bidhaa au huduma iliouzwa
    - **Naira zilizoingia:** ingiza kiasi cha pesa kilichopokelewa
    - **Naira zilizotoka:** ingiza kiasi cha pesa kilichotoka

3. Uliza yeyote kusema kama bidhaa yoyote **ilinunuliwa** au **kuuzwa** tarehe ya Januari 5, 2009. Bidhaa ilinunuliwa (pesa ilitumiwa). Uliza aina ya bidhaa. Ilikuwa kalamu na leja. Uliza bei. Ilikuwa N1,500.

4. Uliza yeyote kutaja maana ya **masalio.** Hi ni tofauti baina ya Naira zilizoingia na zilizotoka. Uliza masalio ni yapi katika mfano wao wa daftari ya fedha taslimu. Ni N900 (N2,400 - N1,500). Waambie kwamba kiasi hiki cha pesa chafaa kiwe kwenye sanduku lao la pesa taslimu.

5. Sasa sambaza picha *daftari tupu ya fedha taslimu*. Pamoja, tutaingiza habari tukitumia mfano fulani. Onyesha karatasi *daftari ya fedha taslimu* ilio na habari utakayoingiza. Soma vitomeo vyote na uwaambie washiriki kuingiza habari hii katika madaftari yao ya fedha taslimu:

   - 8 Jan 2009: mauzo ya chupa 2 za Cypermethrin kwa bei ya N2,600
   - 9 Jan 2009: mauzo ya chupa 1 ya Ultracide kwa bei ya N1,200
   - 9 Jan 2009: kununua kadi ya simu kwa bei ya N500

   Tembelea kila mtu ili kuona kama yeyote ana tatizo kuingiza habari hiyo.

6. Sasa onyesha karatasi lililo na fomu ya daftari tupu ya fedha taslimu (hakikisha kila mtu analiona). Uliza wa kujitolea kuingiza kitomeo cha kwanza na uulize kama kila mtu anakubaliana. Kariri kilichoingizwa ili kila mmoja akisikie. Uliza wa kujitolea mwingine kuingiza habari ya pili, n.k.

7. Sasa uliza wa kujitolea mwingine kukokotoa jumla zote. Matokeo yafaa iwe ifuatavyo:

| **Tarehe** | **Maelezo** | **Naira zilizoingia** | **Naira zilizotoka** |
|---|---|---|---|
| 8 Jan 2009 | Mauzo ya chupa 2 za Cypermethrin | N2,600 | |
| 9 Jan 2009 | Mauzo ya chupa 1 ya Ultracide | N1,200 | |
| 9 Jan 2009 | Kununua kadi 1 ya simu | | N500 |
| **Jumla** | | **N3,800** | **N500** |

8. Uliza yeyote kukuambia **masalio** kutokana na shughuli hii. Hii ni N3,800 - N500, ambayo ni N3,300. Hiki kiasi chafaa kiwe katika sanduku lako la pesa taslimu.

9. Sasa rejelea mfano wa daftari ya fedha taslimu. Hapo tuliona kwamba masalio katika sanduku la pesa taslimu yalikuwa N900. Hii inamaanisha kwamba kiasi hiki kilikuwa bado kiko katika sanduku lako la pesa taslimu ulipofungua duka lako tarehe 8 Januari. Ukizingatia hizi vitomeo vipya na N900 zilioko katika sanduku la pesa taslimu, ni kiasi gani kilicho katika sanduku la pesa taslimu kufikia mwishoni mwa siku/tarehe 9 Januari? Hii itakuwa N900 + N3,800 - N500 ambayo ni N4,200.

10. Sasa eleza **rekodi za ununuzi** kwa njia ile ile uliotumia kueleza daftari ya fedha taslimu. Sambaza picha *mfano wa rekodi ya ununuzi*. Habari ifuatayo huingizwa katika rekodi ya ununuzi:

- **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli ya biashara
- **Ilinunuliwa kutoka kwa:** ingiza jina la kampuni au mtu ambaye ulinunua bidhaa kutoka kwake
- **Maelezo:** eleza bidhaa ulizonunua, pamoja na kiasi
- **Kiasi jumla ulichonunua:** ingiza kiasi jumla ulicholipia
- **Mtindo/namna ya kulipa:** eleza jinsi ulivyolipa. Kama ulilipa kwa kutumia hundi, ingiza nambari ya hundi hiyo. Kama ulilipa kwa kutumia hundi, ingiza nambari ya hundi

11. Pamoja muangalie mfano wa rekodi ya ununuzi na uulize maswali yafuatayo:
    a. Ni kiasi gani cha pesa tulilipa kwa kununua Ultracide? N120,000
    b. Ni bidhaa gani tulilipa kwa kutumia hundi? Aldrex
    c. Ni wapi tulinunua kalamu na leja? katika Pat's bookshop
    d. Ni kiasi gani kwa jumla tulitumia kwa kununua bidhaa katika mwezi wa Januari 2009? N129,500
12. Endelea na **rekodi ya ununuzi ilio tupu** katika njia ile ile ulijadili daftari ya fedha taslimu. Tumia vitomeo vifuatavyo:

    - 09 Jan 2009 kadi ya simu kwa bei ya N500 ililipwa kwa pesa taslimu kutoka kwa mchuuzi wa barabarani
    - 10 Jan 2009 chupa 20 Cypermethrin kwa bei ya N26,000 kwa hundi (nambari 40) kutoka kwa Isaac&Co
    - 11 Jan 2009 chupa 10 za Ultracide kwa bei ya N12,000 kwa muamana ktoka kwa "Golden inputs"

    Jadili ulivyofanya na daftari ya fedha taslimu. Matokeo yafaa yawe ifuatavyo:

| **Tarehe** | **Ilinunuliwa kutoka kwa** | **Maelezo** | **Kiasi jumla cha vilivyonunuliwa** | **Namna/mtindo wa kulipa** |
|---|---|---|---|---|
| 09 Jan 2009 | Mchuuzi wa barabarani | Kadi ya simu | N500 | Pesa taslimu |
| 10 Jan 2009 | Isaac & Co | Chupa 20 za Cypermethrin | N26,000 | Hundi (nambari 040) |
| 11 Jan 2009 | "Golden Inputs" | Chupa 10 za Ultracide | N12,000 | Muamana |
| **VILIVYONUNULIWA KWA JUMLA KATIKA MWEZI WA JANUARI 2009** | | | **N38,500** | |

13. Sasa rejelea lile zoezi la daftari ya fedha taslimu. Ni **vitomeo vipi sawa** tunavyovipata katika daftari ya pesa taslimu na rekodi ya ununuzi? Hii ni **malipo** yaliofanywa kwa **pesa taslimu**. Katika mfano huu, ni kununua kwa kadi ya simu kwa bei ya N500 tarehe ya January 9, 2009. kwa hivyo **malipo yote kwa pesa taslimu yatarekodiwa katika daftari ya fedha taslimu NA na rekodi ya ununuzi**.

14. Endelea na rekodi za mauzo. Habari ya kuingizwa ni:
    - **Tarehe:** ingiza tarehe ya shughuli za kibiashara
    - **Maelezo:** eleza bidhaa ulizouza
    - **Ziliuziwa:** ingiza jina la kampuni au mtu uliemuuzia bidhaa
    - **Bei ya kila moja ya bidhaa:** ingiza bei ya kila bidhaa moja
    - **Kiasi:** ingiza nambari ya bidhaa ulizouza
    - **Kiasi cha jumla:** ingiza jumla ya kiasi cha mauzo
    - **Mtindo/namna ya kulipa:** eleza jinsi bidhaa zilivyolipwa. Kama zililipwa kwa kutumia hundi, ingiza nambari ya hundi hiyo.
15. Uliza maswali yafuatayo:
    a. Ni nini Bw. Adjei alichonunua na kilikuwa kiasi gani kwa jumla? Chupa mbili za Ultracide na 1 ya Snipper kwa jumla ya pesa N1,400.
    b. Ni nani alilipa kwa pesa taslimu? Bw. Adjei
    c. Ni kiasi gani kiliuzwa tarehe 5 Januari? Kwa bei ya N1,500.
    d. Mauzo kwa jumla yalikuwa ya kiasi gani? N4,100.
16. Endelea na **rekodi tupu za mauzo** kwa njia ile ile ulijadili daftari ya fedha taslimu na rekodi za ununuzi. Tumia vitomeo vifuatavyo:

    - 8 Jan 2009: mauzo ya chupa 2 za Cypermethrin kwa bei ya N2, 600 kwa pesa taslimu kwa Bw. Nartey
    - 9 Jan 2009: mauzo ya chupa 1 ya Ultracide kwa bei ya N1,200 kwa pesa taslimu kwa Bw. Abdullai
    - 10 Jan 2009: mauzo ya chupa 2 za Ultracide kwa bei ya N2, 400 kwa muamana kwa Bw. Weja

    Jadili ulivyofanya na daftari ya fedha taslimu na rekodi za ununuzi. Matokeo yafaa yawe ifuatavyo:

| **Tarehe** | **Maelezo** | **Iliuziwa** | **Bei ya bidhaa moja (katika Naira)** | | **Kiasi cha jumla (katika Naira)** | **Namna/mtindo wa malipo** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 08 Jan 2009 | Cypermethrin | Bw. Nartey | N1,300 | 2 | N2,600 | Pesa taslimu |
| 09 Jan 2009 | Ultracide | Bw. Abdullai | N1,200 | 1 | N1,200 | Pesa taslimu |
| 10 Jan 2009 | Ultracide | Bw. Weja | N1,200 | 2 | N2,400 | Muamana |
| **MAUZO YA JUMLA KWA MWEZI WA JANUARY 2009** | | | | | **N 6,200** | |

17. Sasa rejelea lile zoezi la daftari ya fedha taslimu. Ni **vitomeo vipi sawa** tunavyovipata katika daftari ya pesa taslimu na rekodi ya mauzo? Hii ni **mauzo** ambayo tuliopata **pesa taslimu** kutoka kwayo. Katika mfano huu, kwa kuuza Cypermethrin tarehe ya January 8 kwa bei ya N2,600 na Ultracide tarehe ya January 9 kwa bei ya N1,200. **Mauzo yote katika pesa taslimu yatarekodiwa katika daftari ya fedha taslimu NA rekodi za mauzo**.

18. Endelea na **rekodi za wadaiwa na waia**. Habari ya kuingizwa ni:
    - **Tarehe:** hii ndio tarehe ya kuingiza shughuli ya biashara
    - **Jina la mwaia:** ingiza jina la kampuni au mtu aliyepeana muamana
    - **Maelezo:** eleza bidhaa ulizonunua, pamoja na kiasi
    - **Kiasi unachodaiwa:** ingiza kiasi kwa jumla ulichonunua
    - **Kiasi ulicholipa:** Ingiza kiasi ulicholipa tayari
    - **Masalio:** hii ni tofauti baina ya kiasi unachodaiwa na kile ulicholipa tayari

19. Uliza maswali yafuatayo:
    a. Ni nani unayemdai pesa na ni kiasi gani? Sam Kwagi, ni N1,500.
    b. Ni nani anakudai pesa na ni kiasi gani? "Golden inputs", ni N70,000 (ushalipa N50,000 tayari).
    c. Ni nini uliuza kwa muamana? Sacheti 15 za Aldrex.
    d. Ni nini ulinunua kwa muamana? Chupa 100 za Ultracide.

20. Sasa rejelea lile zoezi la **rekodi za mauzo na ununuzi**. Ni nini tulinunua kwa muamana? Chupa 10 za Ultracide kutoka "Golden inputs" kwa N12,000. Na ni nini tuliuza kwa muamana? Chupa mbili za Ultracide kwa Bw. Weja kwa N2,400. Wacha washiriki waongeze habari hii kwa **rekodi zao tupu za wadaiwa na waia.** Matokeo yafaa iwe ifuatavyo:

**Akaunti za kulipwa (Mwaia)**

| Tarehe | Jina la mwaia | Maelezo | Kiasi unachodaiwa | Kiasi ulicholipa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 Jan 2009 | "Golden Inputs" | Chupa 10 za Ultracide | N12,000 | 0 | N12,000 |

**Akaunti za kupokelewa (Wadaiwa)**

| Tarehe | Jina la mdaiwa | Maelezo | Kiasi cha kudai | Kiasi kilicholipwa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 Jan 2009 | Bw. Weja | Chupa 2 za Ultracide | N2,400 | 0 | N2,400 |

Kila mauzo au ununuzi kwa muamana yatakuwa kwa rekodi za mauzo au ununuzi na pia kwa rekodi za wadaiwa na waia.

21. Uliza washiriki kama **mauzo kwa muamana** yanaweza kamwe kuonekana kwa daftari ya fedha taslimu? La, ni kwa wakati tu mteja anapolipa deni lake kwa

kutumia pesa taslimu. Ni vivyo hivyo kwa **ununuzi kwa muamana**. Itaonekana tu kwa daftari ya fedha taslimu wakati utakapolipa kwa kutumia pesa taslimu.

# Malizia

**M**uhtasari: Tumia makaratsi yalio na fomu zilizokamilishwa kupeana muhtasari. Taja aina ya habari inayofaa kuingizwa katika kila fomu.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Pindua makaratasi na uulize wapi tunaandika mauzo kwa pesa taslimu. Hii itakuwa kwa daftari ya fedha taslimu na rekodi za mauzo. Ni wapi tunaandika vinavyonunuliwa kwa pesa taslimu? Katika daftari ya pesa taslimu na rekodi za ununuzi. Ni wapi tunaandika mauzo kwa muamana? Katika rekodi za mauzo na pia rekodi za wadaiwa na waia. Na mauzo kwa hundi? Katika rekodi za mauzo pekee.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi kifuatacho, tutajadili rekodi za bidhaa zilizomo dukani.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.

# DAFTARI YA FEDHA TASLIMU (EXAMPLE)

| Tarehe | Maelezo | Naira zilizoingia | Naira zilizotoka |
|---|---|---|---|
| 04 Jan 2009 | Mauzo ya chupa mbili za Ultracide | N2,400 | |
| 05 Jan 2009 | Kununua kalamu na leja | | N1,500 |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| **Jumla** | | **N 2,400** | **N1,500** |

IFDC

# DAFTARI YA FEDHA TASLIMU (EMPTY)

| Tarehe | Maelezo | Naira zilizoingia | Naira zilizotoka |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| **Jumla** | | | |

## REKODI ZA UNUNUZI (EXAMPLE)

| Tarehe | Ilinunuliwa kutoka kwa | Maelezo | Kiasi jumla cha vilivyonunuliwa | Namna/mtindo wa kulipa |
|---|---|---|---|---|
| 02 Jan 2009 | Isaac & Co | Sacheti 80 za Aldrex | N8,000 | Hundi (nambari 039) |
| 05 Jan 2009 | Pat's bookshop | Kalamu 5 na leja 2 | N1,500 | Pesa taslimu |
| 05 Jan 2009 | Golden Inputs | Chupa 100 za Ultracide | N120,000 | Muamana |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| **JUMLA YA UNUNUZI WA MWEZI WA JANUARI 2009** | | | **N129,500** | |

# REKODI ZA UNUNUZI (EMPTY)

| Tarehe | Ilinunuliwa kutoka kwa | Maelezo | Kiasi jumla cha vilivyonunuliwa | Namna/mtindo wa kulipa |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| **JUMLA YA UNUNUZI WA MWEZI WA** | | | | |

## REKODI ZA MAUZO (EXAMPLE)

| **Tarehe** | **Maelezo** | **Iliuziwa** | **Bei ya bidhaa moja (katika Naira)** | **Kiasi** | **Kiasi cha jumla (katika Naira)** | **Namna/mtindo wa malipo** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 04 Jan 2009 | Ultracide | Mr. Adjei | N1,200 | 2 | N2,400 | Pesa taslimu |
| 04 Jan 2009 | Snipper | Mr. Adjei | N200 | 1 | N200 | Pesa taslimu |
| 05 Jan 2009 | Aldrex | Sam Kwagi | N100 | 15 | N1,500 | Muamana |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| **MAUZO KWA JUMLA YA JANUARI 2009** | | | | | **N3,900** | |

## REKODI ZA MAUZO (EMPTY)

| Tarehe | Maelezo | Iliuziwa | Bei ya bidhaa moja (katika Naira) | Kiasi | Kiasi cha jumla (katika Naira) | Namna/mtindo wa malipo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| **MAUZO KWA JUMLA YA** | | | | | | |

REKODI ZA WADAIWA NA WAIA (EXAMPLE)

## Akaunti za kulipwa (Mwaia)

| Tarehe | Jina la mwaia | Maelezo | Kiasi unachodaiwa | Kiasi ulicholipa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 05 Jan 2009 | "Golden Inputs" | Chupa 100 za Ultracide | N120,000 | N50,000 | N70,000 |
| | | | | | |
| | | | | | |

## Akaunti za kupokelewa (Wadaiwa) (EXAMPLE)

| Tarehe | Jina la mdaiwa | Maelezo | Kiasi cha kudai | Kiasi kilicholipwa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| 05 Jan 2009 | Sam Kwagi | Sacheti 15 za Aldrex | N1,500 | 0 | N1,500 |
| | | | | | |
| | | | | | |

# REKODI ZA WADAIWA NA WAIA (EMPTY)

## Akaunti za kulipwa (Mwaia)

| Tarehe | Jina la mwaia | Maelezo | Kiasi unachodaiwa | Kiasi ulicholipa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

## Akaunti za kupokelewa (Wadaiwa) (EMPTY)

| Tarehe | Jina la mdaiwa | Maelezo | Kiasi cha kudai | Kiasi kilicholipwa | Masalio |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |